

MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu umetayarishwa leo tarehe 24 mwezi 09.mwaka 2025

KATI YA

JOHN JACKSON wa Dar es salaam Tanzania (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MWENYE NYUMBA**”) kwa upande mmoja.

HEROCEAN BAIZHUO TECHNOLOGY TANZANIA LIMITED wa Dar es salaam (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama “**MPANGAJI**” kwa upande mwingine.

NA KWA VILE Mwenye NYUMBA amekubali kupangisha na Mpangaji amekubali kupangishwa sehemu ya nyumba (Chumba) hiyo iliyopo **PWANI** Mtaa wa **KISEMVULE** kata ya **KIMANZICHANA**, Namba ya nyumba **09**, Block **H**, Plot no **9**.

HIVYO BASI Makubaliano hayo yameshuhudia yafuatayo:-

1. MUDA WA MKATABA

Mkataba huu utakuwa wa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 24 Mwezi 09 mwaka 2025 na utamalizika tarehe 24 mwezi 09 mwaka 2028.

2. KODI

Mwenye nyumba amekubali kupangisha na mpangaji amekubali kupangishwa katika sehemu hiyo ya nyumba kwa madhumuni ya kufanya biashara kwa kulipa kodi ya **Shilingi Laki Mbili (200,000)** kwa mwezi mmoja. Wakati wa kutiliana saini mwenye nyumba amekubali kupokea **Tsh Milioni Saba na Laki Mbili Tu (7,200,000)** ikiwa ni malipo ya miaka mitatu.

3. NI WAJIBU WA MPANGAJI KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kutopangisha Mtu mwingine katika nyumba hiyo bila idhini ya Maandishi ya Mwenye nyumba
- (b) Kulipia gharama zote za umeme katika chumba hicho kwa kipindi cha Mkataba.
- (c) Kuweka chumba na mazingira yake katika hali ya usafi na kufanya matengenezo madogo madogo inapobidi na gharama za matengenezo kwa matumizi yake hazitakuwa jukumu la Mwenye nyumba
- (d) Iwapo makubaliano hayo hayataongezwa muda wake, atamkabidhi Mwenye nyumba sehemu hiyo ikiwa tupu.

4. NI WAJIBU MWENYE NYUMBA KUTEKELEZA YAFUATAYO:-

- (a) Kuweka nyumba katika hali nzuri
- (b) Kutombughudhi Mpangaji wa chumba hicho anayesimamia kwa masharti yaliyopo.

5. INAKUBALIWA PIA KUWA

- (a) Endapo Mpangaji atakuwa na Nia ya kuendeleza atawajibika kutoa taarifa ya Maandishi ya mwezi mmoja kabla ya kipindi cha Mkataba kuisha.
- (b) Kama Mpangaji hatakabidhi nyumba hiyo kama walivyokubaliana basi Mwenye nyumba ana haki ya kumtoa kwa kutumia Dalali yeyote bila amri yoyote ya Mahakama.
- (c) Mgogoro wowote utatokea kuhusiana na Mkataba huu, basi mgogoro huo utatambuliwa kufuatana na sheria za nchi.

Mkataba huu umeshuhudiwa na wahusika kwa kutia sahihi zao katika namna na katika tarehe, mwezi na mwaka unaoonekana hapa chini.

**UMESAINIWA na KUTOLEWA na
JOHN JACKSON** ambaye amekubaliwa
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam
Leo 24 mwezi 09 mwaka 2025.

.....
MWENYE NYUMBA

**UMESAINIWA na KUTOLEWA
Na HEROCEAN BAIZHUO TECHNOLOGY TANZANIA
LIMITED** ambaye amekubaliwa
Na ambaye namfahamu hapa Dar es salaam
Leo 24 mwezi 09 mwaka 2025.

.....
MPANGAJI

SHAHIDI;

JINA DANIEL SIMON

SAHIHI 

ANWANI 105069, DSA

KAZI WAKIL

